# Dk. Samia aapisha majaji, awapa maagizo mazito ..Uk.2

tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora

Tanzania BORA

Ni Mimi na Wewe

Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz | ISSN 4256-1873 Toleo Na.09 Tanzania Bora ALHAMISI Januari 23, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100


Tanzania BORA MICHEZO

YANGA YAAPIA MAKUBWA

SIMBA: TUNAOGOPWA AFRIKA

Manchester United kuna vimeo wanane

## UCHAPAKAZI WA DK. SAMIA...

# BoT yanunua tani 2.6 Za dhahabu

>> Ni inayochimbwa nchini yenye thamani ya zaidi ya sh bilioni 570

>> Mavunde asema dhamira ni kuwa nchi 10 zenye hifadhi kubwa ya dhahabu afrika



"Kwa upande wa mapato, Waziri Mavunde amebainisha kuwa, mwenendo wa ukusanyaji wa mrabaha kwa upande wa madini ya dhahabu umeendelea kuimarika na kwamba kuanzia Julai 1, 2024 hadi Desemba 31, 2024, Serikali iliingiza shilingi bilioni 400.22"

>> Mapato yatokanayo na madini ya dhahabu sasa yaongezeka

UK.2



# Bilioni 14.48 Kulipa fidia mradi wa magadi soda Engaruka

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Viwanda na Biashara Mhe.Dkt. Selemani Jafo (Mb) amesema Serikali ya Tanzania inaandika historia katika uendelezaji wa sekta ya viwanda nchini kwa kuzindua zoezi la ulipaji wa fidia kiasi cha shilingi bilioni 14.48 kwa wananchi watakaopisha Mradi wa Magadi Soda uliopo Engaruka, Wilaya ya Monduli Mkoani Arusha.

Ameyasema hayo aliposhiriki Kipindi cha mahojiani cha Jambo Tanzania kinachorushwa na Kituo cha Televisheni cha TBC kilichofanyika Januari 22,2024 katika ofisi za Kituo hicho Dar es Salaam. Dkt.Jafo amesema kati ya kiasi hicho jumla ya shilingi

Inaendelea Uk. 4

# Noti mpya kuanza kutumika Februari mosi

HABARI UK.3

# Wajumbe CCM walipokata mzizi wa fitna

NA MWANDISHI WETU

WAJUMBE wa Mkutano Mkuu Maalum wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) jana walipitisha azimio la kumteua Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea wa nafasi ya urais katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika baadae mwaka huu.

Azimio hilo limepitishwa na Mkutano Mkuu wa CCM ambao ndiyo chombo cha mwisho cha maamuzi ya uteuzi wa mgombea wa tiketi ya urais kupitia chama hicho. Chama hicho pia kimempitisha Dkt. Hussein Mwinyi kugombea Urais kwa upande wa Zanzibar.

Uamuzi huo umefanyika mapema kuliko kawaida, na katika mkutano ambao awali haukupangwa kufanya maamuzi hayo katika ajenda zake. Mkutano huo ulikuwa na ajenda kuu moja ya kupitisha jina la Makamu wa Mwenyekiti (Bara) ambapo mwanasiasa mkongwe Stephen Wasira alipitishwa kushika wadhifa huo jana Jumamosi.

Baadhi ya wajumbe waliokuwa wakitoa michango yao juu ya utekelezwaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM walipendekeza mkutano huo kuwapitisha Rais Samia na Rais Mwinyi kama wagombea wa urais kutokana na maendelea walioyasimamia.

Rais mstaafu Jakaya Kikwete, akizungumza kama mmoja wa wazee wa chama, alisisitiza kuwa CCM ina mamlaka ya kujichagulia mgombea wao kwa wakati wowote. "Hili lipo ndani ya uwezo wetu, kuamua muda wowote, kwamfano wenzetu (wa Swapo) Namibia wao wanafanya uchaguzi kumpitisha mgombea wao mwaka mzima (kabla ya uchaguzi). Sasa na sisi tunaweza kuamua. Jambo la Msingi azimio lipite na tupate ushauri wakisheria ili uendane na matakwa ya tume ya uchaguzi."

Hii ni mara ya kwanza kwa CCM kupitisha wagombea wa nafasi za urais mapema katika mwanzo wa mwaka na katika kikao ambacho ajenda yake mahsusi haikuwa hiyo. Kawaida, maamuzi hayo hufanyika miezi michache kabla ya kuanza kwa kampeni rasmi za uchaguzi mkuu.

Rais Dkt. Samia pia amemteua Katibu Mkuu wa CCM Emmanuel Nchimbi kuwa mgombea mwenza wake katika uchaguzi mkuu utakaofanyika baadae mwaka huu.

Nchimbi ni mwanasiasa mwandamizi na ameshika nafasi mbali mbali ndani ya CCM na serikali yake kwa miongo mitatu iliyopita. Amewahi kushika nafasi ya Waziri wa Mambo ya Ndani katika serikali ya Kikwete na aliteuliwa kuwa balozi na hayati John Pombe Magufuli na kuiwakilisha Tanzania nchini Brazil na baadae Misri.Kwa mujibu wa Rais Dk. Samia, Makamu wa Rais wa sasa Philip Mpango alimuomba apumzike na ameridhia na ndio maana amemteua Nchimbi.

Mpango ataendelea na majukumu yake kama Makamu wa Rais mpaka uchaguzi utakapofanyika, sawia na Nchimbi ambaye ataendelea na majukumu yake ndani ya chama kwa sasa.

Marais wote wawili Dkt. Samia na Dkt. Mwinyi wanamaliza awamu zao za kwanza za uongozi mwaka huu. Na kwa mujibu wa utamaduni wa chama hicho, marais walio madarakani huwa hawapatiwi ushindani katika kupewa tiketi ya kugombea urais kwa awamu ya pili.

Rais Samia aliingia madarakani mwezi Machi 2021 mara baada ya kifo cha aliyekuwa rais wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli. Aliingia madarakani kwa mujibu wa katiba akiwa ndiye mrithi wa urais, kwa nafasi aliyokuwa nayo kipindi hicho ya Makamu wa Rais.



## NCHEMBA: IMF TUTASHIRIKIANA NAYO

NA MWANDISHI WETU

SERIKALI imesema itaendelea kushirikiana na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), na kuhakikisha fedha zote za maendeleo zinazotolewa na Shirika hilo zinatumika kukamilisha azma ya kukuza uchumi wa nchi.

Hayo yameelezwa na Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba jijini Dodoma wakati akimuaga Kiongozi wa Timu ya Wataalam ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa Tanzania, Charalambos Tsangarides, aliyemaliza muda wake baada ya kuhudumu kwa zaidi ya miaka mitatu na nusu.

Alisema Serikali itaendelea kutekeleza dhamira yake ya kuwaletea wananchi maendeleo na kukuza uchumi kwa ujumla kupitia juhudi mbalimbali inazofanya ikiwemo kutafuta fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati.

'Kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, napenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa kujitolea kwako katika kusaidia safari ya maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu, ninawahakikishia kwamba timu yangu itawapa ushirikiano wote unaohitajika, kwa upande mwingine, nina furaha kuwajulisha kwamba tunaendelea vyema na hatua zetu za mageuzi chini ya program mpya ya Serikali ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia dirisha la Resilient and Sustainable Fund (RSF),'' alisema Dkt. Nchemba.

Dkt. Nchemba, mbali na kumuaga Kiongozi huyo wa IMF nchini, alitumia fursa hiyo kumkaribisha Kiongozi mpya anayechukua nafasi hiyo Nicolas Blancher, huku akimuahidi ushirikiano kutoka Serikali ya Tanzania.

''Napenda kuchukua fursa hii kumkaribisha rasmi Nicolas Blancher, kama Kiongozi wetu mpya wa "Mission" kwa Tanzania na tunafurahi kupata nafasi ya kushuhudia mwongozo kutoka kwa mtaalamu mwingine kama tulivyofanya na Kiongozi wa ''Mission''anayemaliza muda wake katika kufanikisha maendeleo yetu endelevu ya kiuchumi'' alisema Dkt. Nchemba.

Kwa upande wake Kiongozi wa Timu ya Wataalam ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa Tanzania, anayemaliza muda wake, Bw. Charalambos Tsangarides, ameishukuru Serikali ya Tanzania kwa ushirikiano mkubwa alioupata wakati akitekeleza majukumu yake nchini.

# NCHIMBI MGOMBEA MWENZA

NA MWANDISHI MAALUM

WAJUMBE wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wameridhia kwa kauli moja kumpitisha Katibu Mkuu wa CCM Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi kuwa mgombea mwenza kwa Mgombea Urais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu wa 2025.

Dkt. Samia Suluhu Hassan alimpendekeza Katibu Mkuu wa chama hicho, Dkt. Emmanuel Nchimbi kuwa mgombea mwenza katika uchaguzi utakaofanyika Oktoba 2025 baada ya Makamu wa Rais, Dkt. Philip Mpango kuomba kupumzika.

Dkt. Nchimbi aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa CCM Januari 15, 2024 katika Kikao cha Halmashauri Kuu ya chama hicho kilichofanyikia Unguja, visiwani Zanzibar.

Dkt.Nchimbi alichukua nafasi iliyoachwa wazi na Daniel Chongolo aliyejiuzulu Novemba 29, 2023.

# MPANGO AOMBA KUPUMZIKA

NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango alimwandikia barua ya kuomba apumzike Umakamu wa Rais ambapo amesema baada ya kutafakari ameridhia ombi hilo.

Lakini kwa sasa Dkt. Mpango ataendelea kuwa Makamu wa Rais hadi utakapofanyika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu 2025.

Akiongea jana kwenye Mkutano Mkuu Maalum wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) jijini Dodoma, Rais Samia alisema, mafanikio yanayoonekana kwa sasa ndani ya Tanzania yalichangiwa kwa kiasi kikubwa ubobecu wa Dkt. Mpango katika suala la uchumi.

“”Dkt. Philip Mpango ndiye Makamu wa Rais miezi ya karibuni hapa amekuja kuniona kuniomba apumzike, ana sababu kadhaa lakini sio za kazi, anasema yeye sasa ana miaka 68 na angependa kuishi zaidi kwahiyo aliomba nimpumzishe.

“Sikumjibu, alipoona nimekaa kimya akaja na barua na sikumjibu, nilipoenda kwenye Kamati Kuu nikawaeleza hiyo hali na kwa pamoja wote tukakubali tumpumzish,” alisema.



*Mwenyekiti Jumuiya Kuu ya Baptist Tanzania Mchungaji Barnabas Ngusa akizungumzia mgogoro kati yao na Kanisa la wabaptist Tanzania uliodumu kwa miaka mitano.*

# MIRADI MIKUBWA YA MAENDELEO KUIMARISHWA

NA MWANDISHI WETU

WATAALAMU wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi nchini wameagizwa kuhakikisha miradi yote mikubwa yenye mvuto wa kibiashara nchini inatekelezwa kwa njia ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kugharamia miradi hiyo.

Agizo hilo limetolewa jijini Dodoma na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha,Jenifa Omolo, kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu Elmaamry Mwamba, wakati akifungua Kikao Cha Kuimarisha Ushirikiano kati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Tanzania Bara kuhusu masuala ya Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP).

Alisema utekelezaji wa miradi kupitia PPP ni sehemu ya kujenga uchumi imara na ni suala ambalo linatekelezwa na nchi nyingi ulimwenguni.

“Msiogope, hata nchi zilizoendelea zinateleza miradi yao kupitia PPP, ukiangalia madaraja na majengo mbalimbali wameyatekeleza kupitia PPP, Sekta Binafsi wakipewa nafasi wanafanya vizuri”, alibainisha Omolo.

Aliwaagiza wataalam hao kukuza uelewa wa dhana ya PPP kwa wadau mbalimbali kwa kuwa bado kuna changamoto ya uelewa wa dhana hiyo pamoja na faida zake.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Zanzibar, Rashid Ali Salim, aliwaagiza wataalam hao kuhakikisha wanayafanyia kazi yale yote waliyokubaliana katika kikao hicho hususani suala la kuwa na mkakati wa pamoja wa kuuza fursa na kuibua miradi ya pamoja ya PPP ili kuimarisha sekta ya PPP nchini.

Naye, Kaimu Kamishna wa Kitengo cha Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), Wizara ya Fedha, Bashiru Taratibu, alisema katika kikao hicho kuna masuala mbalimbali wameazimia kuyatekeleza ikwemo maboresho ya Sheria ili kurahisisha shughuli za PPP nchini hususani katika kutekeleza miradi ya pamoja katika ya Zanzibar na Tanzania Bara.

“Tumejadili kuhusu miradi ya pamoja ambayo Sekta Binafsi inaweza kutekeleza kama mradi wa Daraja la Dar es Salaam hadi Zanzibar, lakini kila sehemu wana Sheria yao ya PPP, kwa hiyo tumekaa kuona namna bora ya kutekeleza suala hilo iwapo mwekezaji atajitokeza,” aliongeza Taratibu.

Alisema Tanzania inahitaji kuwa na Sera au Sheria ya PPP inayoelezea utekelezaji wa miradi ya pamoja kati ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa kuwa suala kama hilo limeshajitokeza katika nchi za Afrika Mashariki ambapo kuna miradi ambayo inaunganisha nchi moja na nyengine na kwasasa tayari kumeshaandaliwa Sera ya PPP ya Afrika Mashariki.

# Jenista: dk. Samia ni wa viwango vya juu

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Afya Jenista Mhagama ametekeleza kwa vitendo maagizo ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Isdor Mpango ya ujenzi wa chuo cha wauguzi kitakachojengwa pembeni ya hospitali ya wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro.

Waziri Mhagama amesema hayo akiwa katika ziara ya siku mbili mkoani Kilimanjaro kwa lengo la kukagua na kuzindua miradi ya sekta mbalimbali ikiwemo ya sekta ya afya katika Wilaya ya Rombo pamoja na wilaya ya Same ambapo amezindua wodi ya wazazi iliyopo katika kituo cha afya Mkuu - Rombo.

"Ndugu zangu Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan haijawahi kupoa, hasa kwenye sekta ya afya, tupo macho kupokea maelekezo na kuyatekeleza, sasa ujenzi wa chuo chetu cha wauguzi utaanza mwezi wa tatu, ili kupunguza tatizo la watumishi ndani ya wilaya, mkoani na Tanzania kwa ujumla," amesema Waziri Mhagama.

Waziri Mhagama amesema tayari Wizara ya Afya imetenga Shilingi Bilioni Moja ili kuanza haraka iwezekanavyo ujenzi huo ambao utakuwa na uwezo wa kuchukua vijana zaidi ya 600 na vijana wa bweni wasiopungua 400.

Aidha, Waziri Mhagama amesema ndani ya miaka mitatu ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali yake imetoa Shilingi Bilioni 82 katika wilaya ya Rombo ili kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo miradi katika sekta ya afya ikiwemo ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya, zahanati pamoja na hospitali.

"Tunaposema Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni wa viwango vya juu tunamaanisha kwa sababu miaka iliyopita Rombo haijawahi kupokea fedha nyingi kiasi hiki na hizo Bilioni 82 ni kati ya Bilioni 956 zilizoletwa katika mkoa huu wa Kilimanjaro, hivyo tuna kila sababu ya kumshukuru Rais kwa kuamua kuibeba Tanzania ukiwemo mkoa wa Kilimanjaro kwa kiwango tofauti," amesema Waziri Mhagama.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu amemshukuru Rais Dkt. Samia kwa mapenzi makubwa ya wananchi wake wa mkoa huo, ambapo katika kipindi cha miaka mitatu mkoa huo umepokea Shilingi Bilioni 956 za maendeleo.

Aidha Waganga Wakuu wa mikoa tisa na Waratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma wa Mikoa wameonesha utayari wao wa shughuli za uibuaji wa wagonjwa wa kifua kikuu kwenye mapango harakishi wa kuwaibua na kuwaweka katika matibabu wagonjwa wa Kifua Kikuu zaidi ya 14000 wakiwemo watoto.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Ahmed Makuwani Januari 8, 2025 wakati akifungua kikao kazi cha Waganga Wakuu wa mikoa, Waratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma wa mikoa na Wataalam wa Wizara ya Afya kujadili utekelezaji wa mpango harakishi wa uibuaji wagonjwa wa Kifua Kikuu.

Mpango huo unategemewa kutekelezwa ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na ngazi ya jamii hususani makundi yaliyo maeneo hatarishi ya maambukizi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu kama vile wachimbaji wa madini, wavuvi, wadungaji sindano, wafungwa na makundi mengine katika mikoa tisa (9) na halmashauri 76 Tanzania Bara.

Dkt. Makuwani amesema Tanzania inaendelea kukabiliana na changamoto ya kuwapata wagonjwa wa Kifua Kikuu na kuwaweka kwenye matibabu ili kuiondoa nchi kwenye kundi la nchi 30 zinazochangia asilimia 87 ya wagonjwa wote wa Kifua Kikuu Duniani.

"Januari 6, 2025 Waziri wa Afya, Mhe. Jenista Mhagama alizindua rasmi mpango wa kitaifa wa kuharakisha uibuaji wa wagonjwa wa Kifua Kikuu katika mikoa tisa (9) ya Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kagera, Mara, Simiyu, Shinyanga, Ruvuma na Tanga na kugawa mashine 185 za ugunduzi wa vimelea vya ugonjwa wa Kifua Kikuu na alitoa maelekezo yanayolenga kuongeza juhudi za uibuaji wagonjwa wa Kifua Kikuu nchini," amesema Dkt. Makuwani.

Dkt. Makuwani amesema, lengo ni kupunguza visa vya Kifua Kikuu kwa 50% na vifo kwa 75% ifikapo 2025 ikilinganishwa na takwimu za mwaka 2015, ambapo kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2023, Tanzania imeweza kupunguza visa vya Kifua Kikuu kwa asilimia 40.

"Tanzania imeweza kupunguza vifo vinavyotokana na Kifua Kikuu kwa asilimia 69 kwa takwimu za mwaka 2023, ambapo lengo ni kupunguza hadi kufikia asilimia 75.



*Picha mbalimbali Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan akiongoza Kikao cha Baraza la Mawaziri kilichofanyika Ikulu Chamwino, Mkoani Dodoma, jana.*

## Ziara za Rais Samia zinavyofungua masoko nje

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk Selemani Jafo amewataka wazalishaji wa asali kwa njia asili kuongeza uzalishaji ili waweze kunufaika na soko la nchini China.Jafo amesema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye sherehe ya uzinduzi wa usafirishaji wa shehena ya asali ya kwanza kutoka Tanzania kwenda nchini China.

Alisema asali hiyo inayozalishwa kwa njia asili inasafirishwa na Kampuni ya East Africa Commercial Logistics Center (EACLC) ikiwa ni matunda ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan nje ya nchi ikiwemo Taifa la China..

Waziri Jafo amesema kupanuka kwa soko la asili nchini China kunatokana na ziara ya Rais Samia nchini China, hivyo kuwataka wazalishaji wa asali kutumia fursa ya soko hilo ili kukuza uchumi wao.

Amewataka wafugaji wa nyuki kote nchini kutumia soko hilo kwa kuzalisha asali safi na salama ili kuwa na soko la uhakika."Nitumie fursa hii kuwaomba wafugaji na wazalishaji wa asali kuchangamkia soko hili kubwa, kwa kuzalisha asali safi na bora,"amesema

Waziri Jafo amesema serikali inaipongeza Kampuni EACLC na serikali ya China kwa kufungua milango ya soko hilo muhimu.Amesema pia soko hilo la asali nchini China litakuwa kichocheo cha utunzaji wa mazingira.

Dk Jafo amesema mkakati wa wizara yake ni kuona Tanzania inakuwa muuzaji mkubwa wa asali duniani na kwamba kupitia soko la China dhamira hiyo inaenda kutumia.Ofisa Mwandamizi kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Karimu Soliambingu amesema wamekuwa wakijenga uelewa wazalishaji wa asali nchini ili waweze kuzalisha asali bora na salama.

Soliambingu amesema wamekuwa wakikusanya sampuli mbalimbali za asali na kupeleka kupima katika maabara ya kimataifa iliyopo Ujerumani, hali ambayo inatoa uhakika wa soko duniani kote.

"TFS imekuwa ikitoa elimu kwa wazalishaji wa asali kuzalisha asali kwenye misitu ili kuepuka kuingiza kemikali, hali ambayo imeongeza ubora na kukubali kwenye soko la dunia," amesema.Amewataka wazalishaji wachangamkie fursa ya soko la China kwa kuongeza uzalishaji hali ambayo itawaongezea kipato.

Ofisa huyo amesema tafiti zinaonesha Tanzania inaweza kuzalisha zaidi ya tani laki moja, hivyo kuwataka wazalishaji kutumia misitu ya TFS kufanya shughuli hiyo.Kwa upande wake Meneja Uzalishaji wa Kampuni ya CDTF Interprises Jackson Ponela amesema uamuzi wa EACLC kupeleka bidhaa zao nchini China umefungua fursa mpya kwenye sekta ya nyuki.

Amesema Tanzania ina asili nyingi, hivyo wanaamini iwapo soko hilo la China litatumia vizuri wazalishaji wa asali watanufaika.



*Katibu Tawala Mkoa wa Tanga, Pili Mnyema (kushoto) akipata ufafanuzi kutoka Mhandisi wa Wilaya ya Kilindi Mhandisi Frank Herman (kulia) wakati wa ziara ya siku moja kukagua ujenzi wa jengo la maabara katika Shule mpya ya Sekondari ya wasichana ya Mkoa wa Tanga iliyopo eneo la Mabalanga Wilayani Kilindi. Picha na Jamal Zuberi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga.*

# SAMIA ATAKA TAA, MAEGESHO DAKAWA, KIBAIGWA

NA MWANDISHI WETU

RAIS Dkt. Samia Suluhu Hassan ameagiza kujengwa kwa maegesho ya malori na taa za barabarani katika miji ya Dakawa na Kibaigwa katika barabara ya Morogoro – Dodoma, ili kupunguza ajali na kukuza biashara katika miji hiyo.

Akikagua barabara hiyo Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega amewaelekeza Mameneja wa Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS ) wa Mkoa ya Morogoro na Dodoma kutekeleza agizo hilo..

"Rais amenielekeza tuhakikishe kwenye barabara kuu nchini kote tunafunga taa za barabarani zinazotumia umeme wa jua (solar) katika miji inayokuwa ili kuongeza usalama, kupunguza ajali na kuimarisha biashara za wananchi wa maeneo hayo," amesisitiza Waziri Ulega.

Waziri Ulega amesema Mameneja wote wahakikishe miji inang'aa kwa taa za umeme jua (Solar), ambazo ni gharama nafuu na kusisitiza kuwa barabara nzuri ni fursa hivyo zikiboreshwa zitachochea maendeleo na kukuza biashara haraka.

"Katika kupunguza msongamano wa magari Morogoro mjini tutajenga barabara wezeshi kati ya eneo la Nanenane - Msamvu na Kihonda - Mkundi tunaomba wananchi mtupe ushirikiano ili eneo hilo liboreshwe," amesisitiza Ulega.

Amesema barabara ya Stesheni hadi Kihonda inajengwa kwa njia nne ili kupunguza msongamano na kuvutia uwekezaji.

Amemtaka Meneja wa TANROADS Mkoa wa Morogoro Mhandisi Alinanuswe Kyamba kuanza ujenzi wa maegesho lenye urefu wa mita 200 na kufunga taa 50 za umeme wa jua eneo la Dakawa na Mhandisi Zuhura Aman wa Mkoa wa Dodoma kufanya hivyo eneo la Kibaigwa ili kupendezesha miji hiyo na kuchochea biashara ili zifanyike pia nyakati za usiku.

Aidha, Ulega amemtaka Meneja wa TANROADS Mkoa wa Dodoma, kuhakikisha ujenzi wa miradi ya dharura unaambatana na uwekaji wa taa za barabarani ili kuimarisha usalama na kupendezesha jiji na kujenga barabara za mchepuko ili kuondoa msongamano wa magari katikati ya jiji la Dodoma.

Kuhusu ujenzi wa miradi ya dharura Waziri Ulega amesema Serikali imetoa Bilioni 54 kwa ajili ya kukarabati madaraja yalioathirika na mvua za el-nino mkoani Morogoro na zaidi ya Bilioni 35 mkoani Dodoma hivyo kuwataka wakandarasi waliopewa miradi hiyo kuongeza kasi ya ujenzi na kufanya kazi usiku na mchana.

Pia Waziri Ulega amemtaka Mkandarasi Estim anaejenga barabara ya Mtanana-Kibaigwa Km 6, kuongeza kasi ili ikamilike kwa wakati. Mradi huo unaohusisha ujenzi wa makalvati makubwa na uwekaji wa taa za barabarani umefikia asilimia 48.9 ambapo zaidi ya shilingi bilioni 26 zitatumika.

"Meneja eneo hili limekuwa changamoto kwa muda mrefu hivyo simamieni kazi hii ifanyike kwa ubora tena usiku na mchana," amesisitiza Waziri Ulega.

Meneja wa Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Dodoma Mhandisi Zuhura Amani amesema Mkandarasi yupo ndani ya muda na ujenzi unaendelea vizuri hivyo amemhakikishia Waziri kusimamia kazi hiyo kikamilifu ili ikamilike kwa wakati na ubora uliokusudiwa.

Ujenzi huo ni sehemu ya mkakati wa Rais Samia Suluhu Hassan kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja na kuweka taa ili yapitike wakati wote wa mwaka kwa usalama na kuchochea biashara katika maeneo ya miji.

## ZIARA YA MKUU WA MKOA WA NJOMBE YAZAA MATUNDA

NA CHRISPIN KALINGA - NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Mhe. Anthony Mtaka, ametembelea kiwanda cha kuchakata mafuta ya parachichi na bidhaa nyingine kinachomilikiwa na kampuni ya Avo Africa Kilichopo Mjini Makambako. Ziara hii ni ishara ya mafanikio makubwa yanayopatikana katika juhudi za kuimarisha uchumi wa mkoa wa Njombe kupitia uwekezaji wa kimkakati.

Kiwanda hicho, ambacho kinatarajiwa kuanza uzalishaji rasmi mwezi Februari 2025, ni mradi mkubwa unaolenga kushughulikia changamoto za wakulima wa zao la parachichi, ambalo limekuwa nguzo muhimu ya uchumi wa mkoa.

"Mwaka 2025 ni mwaka wa suluhisho kwa vilio vya wakulima wa parachichi. Kupitia kiwanda hiki, tunaenda kushuhudia mabadiliko makubwa katika kuongeza thamani ya mazao na kuchochea maendeleo ya kiuchumi," alisema Mhe. Mtaka.

Uwekezaji huu mkubwa ni sehemu ya juhudi za kutekeleza dira ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ya kuimarisha sekta ya uwekezaji nchini.Rais Samia amewahi kusema kuwa, "Tunahitaji kuwakaribisha wawekezaji kwa mikono miwili kwa sababu wao ni chachu ya maendeleo na ajira kwa vijana wetu." Maneno haya yanadhihirika kwa vitendo kupitia kiwanda cha Avo Africa, ambacho kinatarajiwa kuajiri wafanyakazi zaidi ya 400, huku nafasi mpya za ajira zikitarajiwa kutangazwa hivi karibuni.

Mhe. Mtaka alibainisha kuwa mradi huu unaunga mkono jitihada za serikali za kufungua fursa mpya kwa vijana. "Kiwanda hiki siyo tu kwamba kitatoa ajira kwa mamia ya vijana, lakini pia kitapanua wigo wa maendeleo ya mkoa na taifa kwa ujumla. Ni wakati wa wananchi wa Njombe kufaidika moja kwa moja na fursa hizi."

Avo Africa imewekeza teknolojia ya kisasa kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa zinakidhi viwango vya kimataifa, na hivyo kuvutia masoko ya ndani na nje ya nchi. Uwekezaji huu unazidi kuimarisha Njombe kama kitovu cha mazao ya parachichi barani Afrika.Hii ni hatua kubwa inayodhihirisha kuwa Njombe iko tayari kuwa sehemu muhimu ya mabadiliko ya kiuchumi kupitia uwekezaji na ushirikiano wa kimataifa.

# Miradi mikubwa inavyoipaisha Dodoma

NA MWANDISHI WETU



KUKAMILIKA kwa miradi mikubwa ya kimkakati, ustawi wa Jiji la Dodoma, Ujio wa Treni ya kisasa SGR, maendeleo ya biashara na kufunguka kwa shugulki za kiuchumi ni miungoni mwa mambo yanayowaongezea imani Watanzania dhidi ya Serikali yao hususan kiongoizi wake Mkuu Rais Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Awamu ya Sita.

Tayari wananchi wameshaanza kuonja matunda ya miradi iliyokamilika na kutoa huduma katika Mkoa wa Dodoma na wilaya zake kama inayoonyesha hapo chini.

MIRADI ILIYOKAMILIKAI NA KUANZA KUTOA HUDUMA

Katika Wilaya ya Bahi, ukiacha miradi midogo midogo ya wafadhili ikiwemo kukarabati miradi ya zamani ili wananchi wapate maji, lakini ipo miradi mikubwa nayo imekamilika. Ujenzi wa Mradi wa usambazaji maji Chikola. Mradi huo uliopo Kijiji cha Chikola unanufaisha wananchi 3,720, ukiwa umejengwa kwa gharama ya sh. milioni 342,750,000, na ukiwa na vituo vys kuchotea maji (vilula) 16, na tenki lenye ujazo wa lita 30,000.

Mradi wa Maji wa Kisima cha Ndege. Upo Kijiji cha Kisima cha Ndege, wanufaika wakiwa 5,324, ukiwa na vilula 10, tenki la ujazo wa lita 40,000, na umejengwa kwa gharama ya sh. 598,187,737.Mradi wa Maji Lamaiti, utahudumia wananchi 7,194, ukiwa na vilula 23, ujazo wa tenki lita 70,000, na umejengwa kwa gharama ya sh. 835,591,980. Uchimbaji wa kisima na ujenzi wa kituo cha kuchotea maji Kijiji cha Mnase, ambapo wananchi 4,856 wa Kijiji cha Mphangwe watanufaika na mradi huo uliogharimu sh. 477,685,800, ukiwa na vilula 13 na tenki la ujazo wa lita 40,000.

Mradi wa Maji Chifutuka, huo utahudumia wananchi 11,000 wa Kijiji cha Chifutuka, na kuwa na vilula 23, tenki la lita 80,000, ukigharimu sh. milioni 812.6. Mradi wa Maji Kijiji cha Mzogole utahudumia wananchi 6,484, ukiwa na vilula 18, na tenki la lita 40,000, ukijengwa kwa sh. milioni 632.

WILAYA YA CHAMWINO

Wilaya ya Chamwino, ujenzi na upanuzi wa Mradi wa Maji Mlowa bwawani. Mradi huo utahudumia wananchi wa Kijiji cha Mlowa Barabarani wapatao 8,358. Mradi umejengwa kwa gharama ya sh. 213,439,260, huku ukiwa na tenki la lita 90,000. Ujenzi na ukarabati wa mradi wa usambazaji maji katika Kijiji cha Iringamvumi. Mradi huo utanufaisha wananchi wa vijiji vitatu vya Iringa Mvumi Zamani, Iringa Mvumi Mpya na Chita wapatao 8,221, ukiwa na vilula 12, tenki la lita 100,000, na umegharimu sh. 432,618,934.

Ujenzi wa Mradi wa Maji Kijiji cha Dabalo.. Utahudumia wananchi 8,188, na una vilula 18, tenki la lita 150,000, ukigharimu sh. 906,792,586. Mradi wa Maji Kijiji cha Manchali utahudumia wananchi 3,260, vilula 20, tenki lita 135,000 na umegharimu sh. 542,506,260.

WILAYA YA CHEMBA

WIlaya ya Chemba, upo mradi wa uwekaji wa tenki, pampu, mfumo wa umeme wa jua, uwekaji wa mabomba katika vijiji vya Muungano, Chukuruma na Maziwa. Wananchi 8,971wa vijiji hivyo watanufaika kwa mradi huo uliowekwa vilela vitatu na tenki la lita 150,000.

Mradi wa kusambaza maji ya pampu katika Kijiji cha Hania, na ukarabati wa skimu ya usambazaji maji ya Songolo. Wananchi wa vijiji vya Hania na Songolo wapatao 8,282 watanufaika. Mradi una vilula 11, tenki la lita 125,000, na kugharimu sh. 251,950,816. Upanuzi wa ukarabati wa Mpango wa Maji wa Mji wa Chemba, ambapo wananchi 12,084 wa vijiji vya Chambalo na Chemba watanufaika, na wamewekewa vilula viwili na tenki la ujazo wa lita 150,000, na kugharimu sh. 756,701,838.

WILAYA YA KONDOA

Wilaya ya Kondoa. Mradi wa Maji Kwahengwa ambao utahudumia wananchi 3,225 wa vijiji viwili vya Kwahengwa na Sakami, umegharimu sh. milioni 272, ukiwa na vilula 18, na tenki la lita 100,000. Mradi wa Maji Bukulu. Huo unanufaisha wananchi 5,499 ukiwa umejengwa kwa gharama ya sh. 451,572,102, na una vilula saba na tenki la ujazo wa lita 140,000. Mradi Kikore-Mkurumuzi utanufaisha wananchi 5,878 wa vijiji vya Kikore na Mkurumuzi, umewekewa vilula 13 na tenki la ujazo wa lita 150,000.

Mradi wa usambazaji Kijiji cha Bicha, wananchi 2,869 watanufaika, huku kukijengwa tenki la ujazo wa lita 250,000, vilula vitatu, na kugharimu sh. 596,986,317.

WILAYA YA KONGWA

Wilaya ya Kongwa, kuna Mradi wa Maji Kijiji cha Mkoka, wananchi 13,249 watanufaika, baada ya kuwekewa vilula 16, tenki la lita 135,000. Mradi wa Maji Kijiji cha Laikala B utahudumia wananchi 3,882 waliowekewa vilula tisa na tenki la lita 100,000, huku ukigharimu sh. 780,566,436. Usambazaji wa vifaa vya ujenzi vijiji vya Sejeli, Manyata na Laikala A (PbR V), ambapo vijiji vitatu vya Sejeli, Manyata na Laikala A vyenye wakazi 11,357 vitanufaika. Kumewekwa vilula vinne (4), na ujenzi kugharimu sh. 110,020,951. Ujenzi Mradi wa Maji Kijiji cha Mgoroka umegharimu sh. 147,504,830, ukiwekewa vilula viwili na tenki la lita 50,000, na wananchi 1,718 watanufaika.

WILAYA YA MPWAPWA

Wilaya ya Mpwapwa. Ujenzi wa Mradi wa Maji Kidenge-Luhundwa na Mpwanila. Mradi huo utahudumia wananchi 8,897 wa vijiji vya Luhundwa, Kidenge na Mpwanila. Wamewekewa vilula 32, na mradi umegharimu sh. 1,070,460,730.

Ukarabati na uboreshaji wa Skimu ya usambazaji maji ya UVIKO 19 wa Kibakwe. Mradi utanufaisha wananchi 9,878 wa Kijiji cha Kibakwe. Mradi huo uliogharimu sh. milioni 500, una kituo cha kuchota maji kimoja na tenki lenye ujazo wa lita 200,000.

Ujenzi wa Skimu ya Usambazaji maji Kijiji cha Mima, ambapo wananchi 5,557 wa vijiji vya Mima na Igoji II watanufaika kwa kuwekewa vilula 11 na tenki la ujazo wa lita 100,000. Ujenzi wa pampu ya usambazaji maji katika Kijiji cha Iyoma, wananchi 5,712 watanufaika baada ya kuwekewa vilula tisa, tenki la lita 75,000, ukigharimu sh. 409,053,977. Ujenzi wa pampu ya usambazaji maji Skimu ya Kijiji cha Kibakwe, wananchi 3,092 watanufaika kwa kuwekewa vilula tisa na tenki la lita 50,000 na kugharimu sh. 478,604,719.

Ukarabati na uboreshaji wa mradi wa maji Chipogoro ambao utanufaisha wananchi 6,547 wa vijiji vya Chipogoro na Chinoje, na wamewekewa vilula 27 na tenki la lita 50,000, huku mradi huo ukigharimu sh. milioni 87. Ujenzi wa Mradi Kijiji cha Iramba, utanufaisha wananchi 1,222 baada ya kuwekewa tenki la lita 75,000 na vilula vitano. Ujenzi wa pampu ya usukumaji maji katika Kijiji cha Kibagwe iliyojengwa kwa gharama ya sh. 478,604,719, na watu 3,092 watanufaika.

MIRADI INAYOTEKELEZWA 2024/2025

Wilaya ya Bahi. Ujenzi wa Mradi wa Maji Ibihwa utanufaisha wananchi 7,443, na utagharimu sh. 709,317,420. Ujenzi wa Mradi wa Maji vijiji vya Chali Makulu, Chali Isanga na Chali Igongo utanufaisha wananchi 8,678, na unajengwa kwa gharama ya sh. 2,505,608,432. Mradi wa Maji vijiji vya Kigwe na Mapinduzi utahudumia wananchi 8,202, na utagharimu sh. milioni 300.6.

Ujenzi wa Bwawa la Chikopelo linalojengwa kwa gharama ya sh. 2,897,336,937 litanufaisha vijiji vya Chikopelo, Chipanga A, Chipanga B, Chikola, Nghulugano, Chimendeli, Bahi Makuli, Bahi Mjini. Utafiti wa maji chini ya ardhi, uchimbaji wa visima vinane

Inaendelea Uk. 8

## TAHARIRI

# Usimvunje nguvu mkuu wa nchi anapowaza kutukomboa

KUMEKUWA na maneno ya chini chini kwenye mitandao ya jamii juu ya ziara anazofanya Rais Samia Suluhu Hassan kwenye mataifa mbalimbali duniani.

Ziara ambazo zinasaidia kuifungua nchi kimataifa, kuwapa fursa wawekezaji wa ndani kuona upeo wa dunia lakini pia kuweka mazingira mazuri ya kukaribisha wawekezaji wa nje.

Hata hivyo, wapo wanaoumizwa na ziara hizo. Kwa madai hazina maana, zinatumia fedha za walipa kodi bure bila sababu. Wanakwenda watu wengi kuliko ilivyopaswa kuwa.

Ni kauli za wakosaji, ambazo zimejaa hila, ghiba na choyo kisicho na sababu yoyote. Rais Samia Suluhu Hassan amekifanya kile ambacho viongozi wengi waliopata kukalia kiti chake nchini hawakuweza, au walikifanya kwa udogo.

Kitendo cha kuongozana na wafanyabiashara, wanahabari, wasanii, wanamichezo, wanamazingira na watu wa kada mbalimbali katika ziara zake ni upeo wa juu wa kuwafikiria wananchi wake.

Wanapofika huko watu hao ambao baadhi wanajigharamia nauli na malazi, wanatambulishwa kwa diaspora. Wanatambulishwa kwa wafanyabiashara wakubwa au wasanii wakubwa wa nchi anazotembelea Rais Samia.

Hakuna kitu kizuri kama kupata kiongozi anayefikiria hatma ya wananchi wake, angeweza kwenda mwenyewe kimya kimya kisha akarudi kimya kimya na chochote kisitokee. Lakini ameamua kulifanya hili la kuongozana na watu bado wapo wanaomsakama.

Hatumtendei haki, kwa sababu analifanya hili si kwa kushurutishwa na hakuna namna yoyote iwayo kuwa ananufaika na kitendo hiki zaidi ya kuwa wanaokwenda naye ndio wanaonufaika.

Kama hiyo haitoshi, mbali ya ziara za kitaifa anazofanya anapata wasaa wa kufuatilia mikopo na misaada yenye masharti nafuu kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwemo hospitali, miundombinu ya barabara, majengo na taasisi za elimu.

BODI YA UHARIRI
Mhariri Mkuu:
Mhariri Habari za Biashra & Uchumi:
Mhariri wa Habari:
Idara ya Masoko:

MAWASILIANO
JAMVI MEDIA GROUP




*Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ndugu. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa pamoja na viongozi mbalimbali katika Mkutano Mkuu Maalum wa CCM Taifa uliofanyika kwenye ukumbi wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma jana tarehe 19 Januari, 2025.*

## UCHAMBUZI

# Nchimbi -- mshikamano wetu ndio nguzo yetu

ANAANDIKA MSHITITI DK. AHMAD SOVU

KAMA angekuwa mchezaji wa mpira wa miguu wa timu ya Yanga basi Dk. Nchimbi ningemuita Aziz Ki au wa Azam angekuwa Fei toto na kama ni Simba basi ndio Clatous Chama na kama ni Mashujaa basi ndio Reliants Lusajo. Maana amepiga ndipo palipo.

Kupiga huku si kupiga kwa boli hapana, ni kutoa hoja au ukumbusho katika wakati mwafaka na pahala mwafaka.

Akiwa mkoani Singida katika ziara yake ya kwanza kwa mzunguko huu wa pili wa mfululizo wa ziara zake, katibu mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi kwa kinywa kipana kabisa na bila kificho amekemea tabia ya baadhi ya watu wachache kutaka kutugombanisha na kuhubiri chokochoko na kauli za kibaguzi zinazoashiria kuvuruga umoja na mshikamano wetu kama taifa la Tanzania.

Alisema Dk. Nchimbi: “Tusikubali kuacha umoja wetu nawaombeni sana, kama kuna jambo mkienda nyumbani leo na mtu akikuuliza katibu mkuu amesema nini umwambie amesema tusikubali kuacha umoja wetu, tusikubali kugawanywa, tusikubali kufarakanishwa.”

Kauli hii ya Dk. Nchimbi imekuja wakati mwafaka kwani ni kweli zipo bishara za baadhi ya watu kuanza maneno yanayoelekea kuuteteresha umoja wetu.

Watanzania ni wamoja na umoja na mshikamano wetu kwa hakika hauna mbadala.

Umoja na mshikamano wetu ndio umetufikisha katika hatua kubwa ya maendeleo iliyopigwa.

Tumeshuhudia mathalan, katika kipindi cha miaka mitatu tu ya Rais Dk. Samia kumepigwa hatua kubwa za maendeleo.

Uendelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kama vile SGR, umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa miundombinu ya mwendokasi na barabara nchi nzima, ongezeko kubwa la watalii, maboresho makubwa katika sekta ya afya na elimu, maboresho katika sekta ya kilimo, uvuvi, mifugo,michezo, sanaa mawasiliano n.k ni mifano ya umuhimu wa kuwa na umoja, amani na mshikamano kama Taifa.

Hivyo, ni lazima kulinda umoja huu na mshikamano wetu na kuepuka kubaguana kwa misingi ya ukabila, dini, maeneo na matabaka kama alivyosisitiza Dk. Nchimbi kuwa;

“Tanzania lazima iendelee kuwa nchi moja yenye mshikamano, yenye upendo ambayo haibagui watu wake kwa misingi ya ukabila, wala dini wala vyama vya siasa. Wote ni Watanzania, nchi yetu sote tuishi kwa kushirikiana na tupendane.”

Kwa hakika, tunatoa kongole sana kwa Balozi Dk. Nchimbi kwa kukumbusha suala hili muhimu na adhimu kwa Taifa.

Tunatoa mwito kwa viongozi wengine wa serikali, dini, vyama vya siasa na vya kijamii na wananchi mmoja mmoja kuendelea kumuunga mkono Dk. Nchimbi kwa kukumbusha na kuonya kwa yeyote atakayeashiria kutaka kuuteteresha umoja wetu.

# Miradi mikubwa inavyoipaisha Dodoma

Inatoka Uk. 6

(8) vya Nkhome, Bahi Makulu, Lukali, Chipanga A (Sulughai), Nondwa (Chihundiche), Tinai (Isangha), Kongogo (Mkalama), Makanda (Chidete), utanufaisha vijiji vya

Nkhome, Bahi Makulu, Lukali, Chipanga A (Sulughai), Nondwa (Chihundiche), Tinai (Isangha), Kongogo (Mkalama), Makanda (Chidete). na utagharimu sh. 261,640,000.

Ujenzi wa Mradi wa Maji Nagulo Bahi utakaohudumia vijiji vya Bankolo, Mpamantwa, Nagulo Bahi, Iwumba na Ikumbulu utahudumia vijiji sita, na idadi ya watu 29,989 watanufaika, na utagharimu sh. 368,216,000. Mradi wa Maji Asanje utahudumia wananchi 2,887, na utagharimu sh. milioni 450, Mradi wa Maji Isangha utahudumia wananchi 6,493 na utagharimu sh. milioni 539, Mradi wa Maji Nagulo Bahi utahudumia wananchi 9,437, na utagharimu sh. milioni 880, Mradi wa Maji Ilindi wananchi 7,382 watanufaika, na gharama ya mradi ni sh. milioni 770, na ujenzi wa Mradi wa Maji Msisi utahudumia wananchi 6,500 kwa gharama ya sh. milioni 200.

WILAYA YA CHAMWINO

Ujenzi wa Mradi wa Maji Kijiji cha Mheme/Chikola, utanufaisha wananchi 2,589 wa Kijiji cha Mheme, na kugharimu sh. milioni 400.5. Mradi wa Maji Kata ya Mvumi Mission utahudumia wananchi wa vijiji vya Mvumi Mission, Chihembe na Mila, vikiwa na wananchi 8,361 na utagharimu sh. 988,821,460. Mradi wa Maji vijiji vya Handali na Mjelu utahudumia wananchi 5,157, kwa gharama ya sh. 698,201,794, na Mradi wa Maji Kijiji cha Izava (Wali) utahudumia wananchi 1,212, na utagharimu sh. 398,741,316.

Ujenzi wa Mradi wa Maji Nagulo utahudumia wananchi 5,192, na kugharimu sh. 282,848,628, Mradi wa Maji Kijiji cha Haneti utagharimu sh. 920,131,756, na kuhudumia wananchi 7,920, Mradi wa Maji Kijiji cha Mgunga utanufaisha wananchi 2,881, na gharama ni sh. 276,620,980. Mradi wa Maji Kijiji cha Mlowa Barabarani utahudumia wananchi 3,296, na kugharimu sh. 329,382,083, na Mradi wa Maji Kijiji cha Magungu utahudumia wananchi 2,881, na gharama ni sh. 277,616,682.

WILAYA YA CHEMBA

Mradi wa Maji Kijiji cha Machiga- Changamka utahudumia wananchi wa vijiji viwili wapatao 15,649 kwa gharama ya sh. milioni 730. Mradi wa Maji Kijiji cha Chandama utahudumia wananchi wa vijiji viwili, Chandama na Mpendo wapatao 6,669 na utagharimu sh. 555,384,640. Mradi wa Maji Kijiji cha Khubunko utahudumia wananchi 2,786 kwa gharama ya sh. 330,617,919. Na Upanuzi na ukarabati Mradi wa Maji katika vijiji vya Huwekwa, Mlongia, Chinyika, , Kubi, Kwamtoro, Soya, Dalai, Daki, Churuku na Gumbu utahudumia vijiji tisa vyenye wakazi 43,584, na utagharimu sh. 690,342,635.

Utafiti wa maji chini ya ardhi na uchimbaji wa visima 11 katika vijiji vya Cheku A, Ombiri, Mbarada, Madaha, Majengo Mapya, Tumbakose, Sankwaleto, Ndoroboni, Manantu, Binse na Mpendo kugharimu sh. milioni 505,449,637. Mradi wa Maji Kelema- Balai utahudumia vijiji viwili vyenye wakazi 6,659 kwa gharama ya sh. 575,183,014. Usambazaji wa malighafi na bomba na viungo vya bomba katika ukarabati wa Mradi wa Maji Kelema Maziwani na Ovada, utahudumia wananchi 6,713 kwa gharama ya sh. 438,149,820. Mradi wa Maji Kijiji cha Igunga utahudumia wananchi 3,637, na kugharimu sh. milioni 360.

Mradi wa Maji Kijiji cha Kelema Huwekwa, utahudumia wananchi 1,937 kwa gharama ya sh. milioni 365. Mradi wa Maji Kijiji cha Mwailange utahudumia wananchi 7,483 kwa gharama ya sh. 616,364,504. Mradi wa Maji Kijiji cha Mrijo Juu, utahudumia vijiji vitatu vya Mrijo Juu, Olboloti na Mrijo Chini vyenye wakazi 10,725, na utagharimu sh. milioni 800.

WILAYA YA DODOMA

Mradi wa Maji Mapinduzi B utakaogharimu sh. 468,078,000, utanufaisha wananchi 9,383. Mradi wa Maji Mayeto na Hombolo Makulu utahudumia wananchi 8,283 kwa gharama ya sh. 512,230,333. Mradi wa Maji Chikowa utahudumia wananchi wa vijiji vinne vya Chikowa, Bihawana, Iwelewele, na Mapinduzi wapatao 10,693, na utagharimu sh. 568,354,994. Utafiti wa maji chini ya ardhi, na uchimbaji visima viwili Nkulabi na Mahona Makulu, kusafisha kisima na kufanya upimaji wa wingi wa maji utagharimu sh. milioni 84,246,667. Na ukarabati wa Mradi wa Maji Ipala utakaohudumia wananchi 3,516, utagharimu sh. milioni 14.4.

WILAYA YA KONDOA

Ukarabati wa Mradi wa Maji vijiji vya Sauna na Mapinduzi vyenye wakazi 2,234, utagharimu sh. 913,320,252. Ujenzi wa Mradi wa Maji Pahi, utahudumia vijiji viwili vya Pahi na Ikova vyenye wakazi 6,768, na kugharimu sh. 937,877,030. Mradi wa Maji Kijiji cha Kisaki chenye wakazi 4,452 utagharimu sh. 572,085,660. Mradi wa Maji Kijiji cha Baura chenye wakazi 2,219 mradi kugharimu sh. 700,609,870. Mradi wa Maji Kijiji cha Kikilo Kati kuhudumia wananchi 4,444 kwa gharama ya sh. 396,712,504. Mradi wa Maji Mauno kujengwa kwa gharama ya sh. 489,195,353, na kunufaisha wananchi 7,574. Mradi wa Maji Soera kujengwa kwa gharama ya sh. 278,390,110, na kuhudumia wananchi 2,713.

Ujenzi wa Mradi wa Maji Sambwa kuhudumia wananchi 29,243 wa vijiji sita vya Sambwa, Idindiri, Keikei, Ihari,Keikei Tangini na Ikengwa, na kugharimu sh. 3,155,324,424. Bwawa la Itaswi- Kisaki kugharimu sh. 5,700,884,713. Mradi wa Maji Kwamafunchi kuhudumia wananchi 2,219, na kugharimu sh. 809,537,820. Mradi wa Maji Madege kuhudumia wananchi 3,124, na kujengwa kwa gharama ya sh. 470,397,532. Mradi wa Maji Masawi kugharimu sh. 1,160,433,839. Na utaweza kuhudumia wananchi wa vijiji vinne vya Masawi, Bereko, Lembo na Alagwa wapatao 10,806.

Ujenzi wa Mradi wa Maji Kikore na Mkurunzi, utahudumia wananchi 4,413, na utagharimu sh. 889,241,348. Mradi wa Maji Bambare kuhudumia wananchi 3,692, na utagharimu sh. 1,270,494,630. Mradi wa Maji Itundwi kuhudumia wakazi 3,592, na gharama ya mradi ni sh. 784,159,091. Mradi wa Maji Hachwi, wananchi 2,470 kunufaika, na utagharimu sh. 803,911,272. Mradi wa Maji Mulua una wakazi 6,958, na utagharimu sh. 872,866,209. Mradi wa Maji Kilimani utagharimu sh. 706,556,681, na utanufaisha wananchi 4,316.

Ujenzi wa Mradi wa Maji wa Mji wa Kondoa utanufaisha wananchi 24,674 kwenye vijiji saba vya Mnarani, Maji ya Shamba, Iboni, Chemchemi, Miningani, Kichangani na Ubembeni, na utagharimu sh. 4,094,604,597. Mradi wa Maji Tampori, Gubali na Choka utahudumia wananchi 5,316 na utagharimu sh. 1,025,725,050. Ujenzi wa miradi midogo (Point Source) katika vijiji vya Matangalimo, Nanakwi B, Ikengwa, Mkundulu na Hurui kuhudumia wananchi wa vijiji vitano na utagharimu sh. 222,335,159.

Ujenzi wa miradi midogo (Point Source) katika vijiji vya Masange, Ntomoko, Filimo, Changaa, Changaa Sekondari, Madege, Mitati, Salanka, Itundwi na Haubi. Wananchi wa vijiji 10 watakaonufaika, na mradi utagharimu sh. 184,234,782. Ujenzi wa vichoteo vinane katika vijiji vya Munguri, Dumi, Hurumbi, Msui na Chora, wananchi wa vijiji vitano watanufaika, na utagharimu sh. 221,299,277. Mradi wa Maji Kisesa Sauna na Kikore, wananchi wa vijiji viwili wapatao 5,878 kunufaika, na utagharimu sh. 184,234,782.

WILAYA YA KONGWA

Mradi wa Maji Masinyeti ambao utagharimu sh. 797,192,950, na kunufaisha wananchi 3,546. Utafiti na uchimbaji wa visima tisa kwenye vijiji vya Silale, Chiwe, Mahutya, Chang'ombe, Ngoma, Nyerere, Magereza (Manyata), Wenzamtima, Muungano (Songambele). Mradi utagharimu sh. 436,545,000.

Utafiti na uchimbaji wa visima 16 kwenye vijiji vya Lengali, Kinangali, , Bwawani, Njoge, Masenha, Silwa, Mbande, Idido, Mangweta, Ihanda, Lobilo, Soiti, Chitego, Wangazi, Matanga na Mgoloka. Mradi huo utagharimu sh. 735,199,472. Mradi wa Maji Chinanjilizi, utahudumia wananchi 1,502, na utagharimu sh. 490,488,617. Mradi wa Maji vijiji vya Chamkoroma na Makole utahudumia wananchi 7,235, na utagharimu sh. 542,100,904. Mradi wa Maji Ijaka kuhudumia wakazi 4,004, na utagharimu sh. 417,305,904. Mradi wa Maji Mangweta unajengwa kwa gharama ya sh. 68,333,800, na wananchi 2,143 watanufaika.

Ujenzi wa Mradi wa Maji Matanga na Ngutoto utanufaisha wananchi wa vijiji viwili wapatao 6,018, na unatekelezwa kwa gharama ya sh. 95,934,000. Mradi wa Maji Songea mbele na Masenha unaojengwa kwa gharama ya sh. milioni 556.8, utanufaisha wananchi 17,823. Na Mradi wa Maji Mtanana B, utahudumia wananchi 4,088, na unajengwa kwa sh. 103,983,378.

WILAYA YA MPWAPWA

Ujenzi wa Mradi wa Maji Chinyika- Mlunduzi. Utahudumia wananchi wa vijiji viwili wapatao 8,176, na utatekelezwa kwa gharama ya sh. 967,668,470. Mradi wa Maji Kijiji cha Igoji I. Utahudumia wananchi 6,183, na utagharimu sh. 430,553,311. Mradi wa Maji Lupata- Makutupa, utahudumia wananchi wa vijiji viwili wapatao 9,286, na utagharimu sh. 2,527,100,461. Mradi wa Maji ambao utahudumia wananchi wa vijiji vinne vya Pwaga, Munguwi, Maswala na Itende wapatao 18,599, utagharimu sh. 4,303,281,669.

Ujenzi wa miundombinu ya tenki la maji na ofisi Mradi wa Maji Mtera, kunufaisha wananchi 6,476, na utagharimu sh. 1,783,973,588. Mradi wa Kijiji cha Gulwe utanufaisha wananchi 5,832, na utagharimu sh. 628,683,958. Upanuzi wa Mradi wa Maji kutoka Pwaga kwenda Idaho. Utahudumia wananchi 1,415, na kugharimu sh. milioni 356. Upanuzi wa Mradi wa Maji Lupeta- Makutupa kwenda Kijiji cha Inzomvu, utahudumia wananchi 7,349, na unajengwa kwa sh. milioni 370. Mradi wa Maji Berege Sekondari unajengwa kwa sh. milioni 156 na utanufaisha watu 1,000.

Ujenzi wa Mradi wa Maji Kijiji cha Mwanawota, unatekelezwa kwa sh. milioni 650, na utahudumia wananchi 3,970. Mradi wa Maji Kijiji cha Chaludewa unajengwa kwa gharama ya sh. milioni 450, na utahudumia wananchi 3,472. Mradi wa Maji Kijiji cha Mzogole, wananchi 2,107 watanufaika, na unajengwa kwa gharama ya sh. milioni 180.

Ukarabati wa Mradi wa Maji Kijiji cha Chinyanhuku unaotekelezwa kwa sh. milioni 155, utahudumia wananchi 4,445. Upanuzi wa Mradi wa Maji Luhundwa Chang'ombe, unajengwa kwa sh. milioni 200, na utahudumia wananchi 1,456. Mradi wa Maji Pandambili, unatekelezwa kwa sh. milioni 210, na utanufaisha wananchi 1,212. Upanuzi wa Mradi wa Maji Kisokwe- Idilo Mazae, utahudumia vijiji vitatu vyenye wakazi 6,662, na utagharimu sh. milioni 864. Na utafiti wa maji ardhini na uchimbaji wa visima virefu vijiji vya Chimaza, Nana na Mkanana Chibwegere. Utagharimu sh. milioni 135.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshiriki maadhimisho ya kilele cha Miaka 61, ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yaliyofanyika katika uwanja wa Gombani, wilaya ya Chakechake, mkoa wa Kusini Pemba, Zanzibar leo tarehe 12 Januari, 2025.*








*Mgeni Rasmi wa maadhimisho hayo alikuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi.*

# Kupitishwa kwa Dk.Samia Suluhu kugombea urais ni uthibitisho wa uwezo wa mwanamke

NA MWANDISHI WETU



DK.SAMIA Suluhu ndiye mgombea Urais wa CCM mwaka huu.Ni yeye baada ya Mkutano Mkuu wa CCM kumpitisha kupeperusha bendera ya chama hicho kwenye uchaguzi Mkuu wa Rais,Wabunge na Mdiwani utakaofanyika Oktoba mwaka huu.

Jahazi la CCM litaongozwa na yeye Dk.Samia kwa kusaidiana na Dk.Emmanuel Nchimbi. Kupitishwa kwa Dk.Samia ni ishara ya kukubalika kwake katika katika kutekeleza ilani ya CCM na kuiongoza vyema serikali yake katika kuwaletea maendeleo Watanzania.Hili halina ubishi.

Nani anasema anaweza kuthubutu kusema wanawake hawawezi? Mimi ninasema wanawake wanaweza, tena wanaweza kile ambacho wanaume wanaweza hata kuzidi.Kupitishwa kwa Dk.Samia ni salaam kubwa kwa watu wenye kuamini katika mfumo dume.

Ndiyo, Wanawake wamejaaliwa uwezo mkubwa katika kutekeleza majukumu mazito kabisa katika jamii. Mtazamo hasi wa jamii juu ya uwezo wa wanawake umewadunisha wanawake kwa karne nyingi na hata kuonekana kuwa hawawezi.

Jamii hususani jamii ya kiafrika,kwa karne nyingi imeaminishwa kuwa wanawake ni wasaidizi tu tena ni wasadizi wa shughuli za nyumbani na kwenye nafasi ndogo ndogo za uongozi. Kama nilivyotanguliza hapo juu hali hiyo imetokana na mtazamo hasi wa jamii juu ya uwezo wa mwanamke katika nyanza za uchumi na uongozi.

Mtazamo huo hasi ungalipo miongoni mwetu hata sasa. Namna nzuri ya kuondoa mtazamo huo hasi na kuachana na fikra hizo mgando, ni kuwatazama viongozi wanawake na namna walivyoweza kufanya makubwa yaliyoigusa jamii na kuiondoa katika kero ikiwemo umaskini wa kipato.

Tanzania tumepiga hatua kubwa katika kuthibitisha kuwa wanawake wanaweza tena wanaweza sawa sawa na hata kuzidi wanaume. Tunao viongozi wengi wanawake ambao wanafanya vizuri katika sekta za uongozi na uchumi.

Makala hii kipekee itaangazia utawala wa Rais wa awamu ya sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, Mwanamama shupavu na namna alivyobadili mtazamo hasi wa jamii juu ya kile jamii ilichokuwa inakiamini kuwa wanawake hawawezi.

Nafasi ya urais sio ya mchezo mchezo, ni nafasi kubwa ambayo kwa hapa nchini Rais ndiye Amiri jeshi Mkuu wa majeshi ya Ulinzi na usalama. Rais ni muhimili wa nchi na ndiye mwenye dhima kubwa ya kuhakikisha nchi inakuwa salama na wananchi si tu wanashiriki katika shughuli za ujenzi wa Taifa, bali shughuli hizo zinakuwa na tija na zinawainua watu hao kiuchumi na kuwaondoa kwenye lindi la umaskini.

> **Rais Samia ametatua changamoto nyingi ambazo huenda ziliihitaji zaidi ya miaka mitano. Tanzania sasa inafunguliwa katika diplomasia na mahusiano ya kimataifa.**

Makala hii itaangazia mazuri aliyoyafanya Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kipindi cha miaka minne madarakani ambayo yanathibitisha uwezo mkubwa aliokuwa nao mwanamke katika nyanza za uongozi.

Machi 19 mwaka huu, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan alitimiza miaka minne ashike hatamu za kuiongoza Tanzania. Hatamu hiyo ya uongozi aliyoichukua kutokana na kifo cha Rais wa awamu ya tano, John Pombe Magufuli, kilichotokea Machi 17, 2021.

Samia alikuwa makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muda wa miaka mitano ambapo alionesha uwezo mkubwa wa kiongozi.

Kutokana na umadhubuti na uthabiti wa utendaji wa Samia, akiwa makamu wa Rais, Rais Magufuli alimpendekeza tena kuwa mgombea mwenza wake kwa nafasi ya Urais kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 na hatimae kuwa makamu wa Rais mpaka pale Rais Magufuli alipofariki dunia.

Samia aliapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano akiwa ni mwanamke wa kwanza kushika wadhfa huo hapa nchini kwetu na katika ukanda huu wa Afrika Mashariki. Rais Samia anaingia kwenye historia ya Tanzania kwa kuwa Makamu wa kwanza wa Rais mwanamke na Rais wa kwanza mwanamke.

Ukweli ni kwamba Rais Samia licha ya kuwa ni mwanamke, ameimudu vyema nafasi hiyo ambayo aliipokea katika kipindi ambacho hakuwa amefanya maandalizi ya kuchukua dhamana hiyo kubwa. Kipindi ambacho Taifa lilikuwa linabubujikwa na machozi na kutawaliwa na hali ya sintofahamu iliyotokana na huzuni ya kuondokewa na Rais aliyekuwa madarakani.

Lakini kwa ushupavu mkubwa Rais Samia aliweza kulituliza Taifa na kuondoa sintofahamu zote ambazo watanzania walikuwa nazo juu ya hatma ya uongozi wa nchi yao.

Rais Samia ameonesha uwezo mkubwa wa kiuongozi unaojali misingi ya utu na usawa,uongozi usio na upendeleo wa kikanda wala wa kitabaka. Kubwa zaidi ameweza kulituliza Taifa na kulibakiza kwenye reli ya amani na utulivu ambazo ndizo tunu zetu za Taifa.

Ukweli ni kwamba uongozi wa Rais Samia umetegua kitendawili cha mwanamke kutoka kwenye kuonekana kuwa hawezi na kuidhihirishia jamii kuwa mwanamke anaweza sawasawa na mwanaume.

Rais Samia amedhihirisha kuwa mwanamke anaweza kushika nafasi yoyote ya uongozi kwenye jamii na akakata kiu ya wanajamii hao, kiu ya maendeleo na pakawepo na amani na utulivu.

Uongozi wa Rais Samia katika kipindi hiki cha miaka minne umeonesha umahiri mkubwa katika kuwahudumia watanzania na kuwareshea matumaini makubwa katika kutatua kero zilizokuwa zinawakabili. Kero kama vile upatikanaji wa huduma bora za elimu, afya, miundombinu, maji, siasa, na uongozi.

Ni ukweli usiopingika kuwa Rais Samia kwa muda alikokaa madarakani amezigusa nyanza hizo kwa namna ambayo inawatia matumaini watanzania wa hali ya chini na kuona kuwa wamepata mkombozi wa kweli wa masahibu yaliyokuwa yakiwasibu kwa miaka nenda rudi.

Ukweli ni kwamba huduma duni za msingi katika jamii watu wa hali ya chini ni wahanga wakubwa kwa kuwa hawana uwezo wa kugharamia kupata huduma hizo. Unapozungumzia ubovu wa barabara, upatikanaji duni wa maji, ukosefu wa huduma za afya za uhakika, watu wa daraja la chini au kama tulivyozea kuwaita makabwela ndio wahanga namba moja.

Mathalani katika sekta ya elimu, Rais Samia eneo la elimu ameligusa kwa namna ya pekee ambayo anastahili pongezi. Sera ya elimu na marekebisho yaliyofanywa juu ya zuio la mtoto wa kike aliyepata ujauzito kurejea shuleni ni hatua ambayo imelenga kumkomboa mtoto wa kike na jamii kwa ujumla kwani, kumueleimisha mtoto wa kike ni kuielimisha jamii.

Hatua ya Rais Samia, kufanikisha ujenzi wa madarasa 15,000 nchi nzima, shule za msingi na sekondari, ni hatua ambayo imelenga kuinua sekta ya elimu na imemuondolea mzigo fukara wa Tanzania na imethibisha umathubuti wa Rais Samia katika kupamba na ujinga kwa kuhakikisha kuwa Taifa Tanzania linakuwa na watu walioelimika ambao watamudu kupambana na changamoto za nyakati.

Kwa upande wa huduma za afya ni wazi kuwa Rais Samia madarakani, huduma za afya kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali za rufaa zimeboreshwa kwa kiwango cha kutia matumaini.

Sambamba na hilo ujenzi wa vituo vya afya unaoendelea nchi nzima ni mwendelezo wa tija kubwa kwa wananchi wa Tanzania. Kila mmoja wetu ni shahidi juu ya adha wanazozipata Watanzania hususani wa vijijini kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za afya. Idadi ya wanawake waliofia njiani kuelekea kupata huduma za afya wakati wa kujifungua ni kubwa pia. Hivyo tunaamini kuwa kasi ya uboreshaji wa huduma za afya ambayo Rais Samia ameionesha inakwenda kuwa mkombozi mkubwa kwa afya ya watanzania.

Ukweli ni kwamba uongozi wa Rais Samia unaaondoa shaka ya uwezo wa mwanamke katika nyanja za uongozi, kwani kipimo kikubwa cha umathubuti wa kiongozi ni namna anavyotatua changamoto za watu anao waongoza.

Rais Samia ametatua changamoto nyingi ambazo huenda ziliihitaji zaidi ya miaka mitano. Tanzania sasa inafunguliwa katika diplomasia na mahusiano ya kimataifa.

Uongozi wa mwanamama huyu shupavu umerejesha mahusiano mazuri na nchi wahisani na nyingine ambazo manufaa yatokanayo ni kuongeza wawekezaji katika sekta ya uchumi ambapo wananchi tutanufaika kwa kupata ajira na fursa nyingine za kibiashara.

# Uvunaji magogo, mbao unavyoharibu mazingira na kuteketeza misitu ya asili



INHAMBANE, MSUMBIJI

SHIRIKISHO la Wavunaji na Wafanyabiashara ya Magogo na Mbao la Msumbiji (FEDEMOMA), limelipongeza Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) kwa kulisaidia kuboresha usimamizi wa misitu kwa kupitia sekta binafsi.

FEDEMOMA inaundwa na jumuiya 16 za wavunaji na wafanyabiashara wa magogo na mbao kutoka majimbo tisa ya nchi hii, zile ambazo zinawakilisha takribani vyama 600 vya msingi vyenye wajasiriamali wadogo na wa kati (MSMEs), na pia vinajumuisha wamiliki wa vitalu vya miti pamoja na wauza mkaa wasiopungua 100.

Katika hatua yake ya kuhamasisha kuwepo kwa mdahalo wa wazi unaohusisha watu wote na sekta binafsi, shirikisho hilo linalenga kupanua wigo wa usimamizi wa misitu hapa nchini.

Malengo yake mengine ni kuvifanya vyanzo vya uwepo wa misitu kuwa endelevu, kupunguza ukataji ovyo wa miti na kuimarisha fursa za uchumi misitu kwa kufuata sheria, kusimamia mazingira na uwajibikaji katika biashara ya magogo na mbao.

RAIS WA SHIRIKISHO

Kuanzishwa kwa FEDEMOMA kulitangazwa rasmi wakati wa kufungwa kwa warsha iliyohusu mradi wa "Kuimarisha Usimamizi wa Misitu kwa Kuongeza Uwakilishi wa Sekta Binafsi".

Kwa kutumia Sheria ya Huduma, Usimamizi na Biashara ya Mazao ya Misitu (FLEGT) ya Shirika la Chakula na Kilimo Duniani – Umoja wa Ulaya (FAO – EU), FAO iliamua kuuunga mkono Umoja wa Wafanyabiashara ya Mbao wa Msumbiji, maarufu kwa kifupi cha AMOMA.

"FEDEMOMA itawapa wanachama wa umoja huu fursa ya uzalishaji wenye tija ili kufikia malengo yao katika upande wa kwanza, na pia itawasaidia wavunaji wa magogo na wafanyabiashara ya mbao, mafundi mchundo pamoja na watengenezaji wa bidhaa zitokanazo na miti katika upande wa pili", anasema Rais wa Shirikisho hilo, Jorge Chacate.

HATUA ZA HARAKA

Msumbiji ni moja kati ya nchi zenye utajiri mkubwa wa misitu ya asili barani Afrika, ile ambayo inachukua asilimia 40 ya ardhi yake yote.

Wakati hali ikiwa namna hiyo, ukataji miti nchini humo unaelezwa kuwa ni hekta 267,000 kwa mwaka, kwa mujibu wa taarifa ya taasisi inayoitwa kwa kifupi cha MITADER.

Kibaya zaidi ni kuwa ukataji huo umekuwa ukifanyika kinyume cha sheria, na pia unasababisha kuwepo uharibifu mkubwa wa mazingira. Kutokana na hali hiyo, hatua za haraka za kuidhibiti zinatakiwa zichukuliwe kwa kuanza na maeneo ambayo yameathirika kwa kiwango kikubwa zaidi, njia zote zinazotumika kupitishia magogo na mbao hizo pamoja na kupunguza utumiaji wa mkaa kwa wakazi wa mijini.



UKAGUZI NA UDHIBITI

Wakati hayo yakiendelea, moja kati ya changamoto zinazoikabili sekta binafsi katika suala hilo la ukataji na biashara ya magogo na mbao hapa nchini ili pamoja na mambo mengine, kufikia lengo la kusimamia vizuri misitu ikiwa miongoni wadau muhimu na wakuu ni "ukosefu wa muunganiko na mfumo wa uwakilishi".

Ndiyo maana FEDEMOMA ikajitosa kuja na mdahalo wa wazi kuhusu misitu na ushirikiano baina ya sekta binafsi na serikali ili kuongeza uelewa wa usimamizi, kuelimisha faida za kiuchumi zitokanazo na mazao ya misitu na njia bora zaidi za kuwa na uhifadhi endelevu wa raslimali hiyo ya asili.

Kana kwamba haitoshi, shirikisho hilo pia limepanga kuongeza ushirikiano baona yake na sekta binafsi katika kukuza uwezo wa usimamizi endelevu wa misitu, na pia katika kuchangia uimarishaji wa ukaguzi na udhibiti wa mavuno na biashara ya magogo na mbao.

WAFADHILI WAKUU

Kuanzia mwaka 2016 hadi sasa, Mpango wa FAO-EU FLEGT umesaidia miradi minne tofauti nchini Msumbiji, yote katika ujumla wake ikigharimu dola 400,000 za Marekani au shilingi 1,037,600,000 za Tanzania.

Lengo la kufanya hivyo ni kupambana na uvunaji wa misitu usiozingatia sheria kwa kuitumia sekta binafsi, kukabiliana na uharibifu wa mazingira utokanao na ufyekaji ovyo wa miti kwa ajili ya kuvuna magogo na mbao na kusaidia vikundi vya ushirika kuhusu usimamizi na uratibu wa maliasili ya misitu.

Mpango wa FAO-EU FLEGT umeenea sehemu mbalimbali duniani na umekuwa pia ukisaidia masuala ya kiufundi kuhusiana na hifadhi ya misitu ya asili. Wafadhili wakuu wa mpango huo ni watatu ambao ni Jumuiya ya Ulaya (EU), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa wa Misaada la Sweden (SIDCA) na Idara ya Kimataifa ya Maendeleo ya Uingereza, maarufu kwa kifupi cha DIDUK.

# Matajiri ambao hawakuionea aibu fedha

NA CHARLES CHARLES

INAELEZWA kila mtu anazaliwa tajiri lakini pia masikini. Utajiri au umasikini wake unategemea na mazingira anayokulia, lakini inategemea zaidi na yeye mwenyewe. Wapo matajiri wengi duniani ambao hawakuzaliwa matajiri. Walitengeneza utajiri wao kwa kupitia maisha ya kawaida kabisa ambayo kila mtu ama wengi wa watu wanayaishi.

Kwa mujibu wa Forbes wapo mabilionea zaidi ya 2,700 duniani lakini wengi wao walianza kufanya kazi za kawaida kabisa ambazo usingedhani kama wangeweza kuwa mabilionea.

1: Jeff Bezos

Huyu ni mmiliki wa kampuni kubwa duniani ya Amazon ambaye kwa sasa ndio tajiri namba mbili duniani. Lakini Bezos kufika kuwa bilionea namba mbili duniani safari yake imetokea mbali. Kazi yake ya kwanza alikuwa mpishi tu, akiandaa vyakula kama baga katika kampuni ya McDonald. Alikuwa na umri wa miaka 16 tu wakati akifanya kazi hiyo na kulipwa dola $2.69, kwa saa moja.

Mbali na Amazon pia anamiliki The Washington Post aliyoinunua mwaka 2017.

Disemba 2013, Bezos alishika vichwa vya habari kwa kuanzisha majaribio aliyoyaita “Amazon Prime Air,” ambayo ni utumiaji wa ndege zisizokuwa na rubani kupeleka huduma kwa wateja wake. Ndege hizo zinaweza kubeba vifurushi vyenye uzito wa mpaka kilo 2.5 na zinaweza kufika umbali wa mpaka maili 10 kutoka ofisi za usambazaji za Amazon.

2: Elon Musk

Amekulia Amerika Kusini baadae akahamia Canada akiwa na umri wa miaka 17 na kuanzia kazi ya kawaida kabisa kama Mhandisi wa program za Kompyuta. Ilikuwa mwaka 1983 na alikuwa akiuza michezo ya kompyuta na kulipwa dola 500 kwa mwezi. Mwezi Januari 2021, Musk aliripotiwa kumpiku Jeff Bezos kama mtu tajiri zaidi duniani.

Lakini sasa ni tajiri akiajiri maelfu ya watu kupitia makampuni zake za Tesla na SpaceX zinazotengeneza roketi, magari ya umeme, umeme wa jua na mabetri.

Utajiri wake ulianza kukuwa kwa kasi akiwa na miaka kati ya 25 na 30, akianza kwa kuiuza kampuni yake ya mwanzo mwanzo tu ya Zip2 kwenda kuwa sehemu ya Compaq Computers. Wazazi wake walitengana akiwa na miaka 10 na hapo akanza kupenda masuala ya kompyuta.

Alijifunza mwenzewe namna ya kutengeneza program za kompyuta, na akiwa na umri wa miaka 12 tu akauza program yake ya kwanza, ilikuwa ya mchezo ya kompyuta (game) iliyoitwa Blastar, safari ya utajiri ikaanzia hapo, alikuwa akitengeza na kuuza kwa bei chee kidogokidogo baadae ujuzi wake ukampa fedha na kuwa mmiliki wa kampuni kubwa duniani ya masualoa ya teknolojia.

3: Bill Gates

Bill Gates ni bilionea anayefahamika sana na mmiliki wa kampuni ya Microsoft. Amekuwa na mchango mkubwa katika bara la Afrika kupitia taasisi yake na mkewe ya Bill & Melinda Gates Foundation ambayo imekuwa ikisaidia masuala mbalimbali ya kijamii.

Ameongoza pia kwenye zoezi la kusaidia chanjo ya polio kwa watoto barani Afrika. Lakini hakuanza kama bilionea, alianza kama mfanyakazi wa kawaida tu kwenye kampuni iliyokuwa ndogo ya TRW, alikuwa mtengeza program za kompyuta wa kampuni hiyo.

Bill Gates alikacha shule akiwa mdogo tu akiwa na rafiki yake wa utotoni Paul Allen na kuamua kuanzisha Microsoft. hakuwa anaeleweka na familia yake, lakini aliamini katika fikra zake na kwa kuanza kidogokidogo akajikuta anakuwa na kutengeneza utajiri wa kutosha.

4: Warren Buffet

Warren Buffet, mfanyabiashara na bilionea mkubwa Marekani, alianza kazi ya kusambaza magezeti tu mtaani, majumbani na maofisini akifanya kazi hiyo ya kusambaza magazeti ya The Washington Post na kulipwa kama dola 175 kwa mwezi.

Lakini sasa ni bilionea wa kutupwa akiwa mkurugenzi mtendaji wa makampuni ya Berkshire Hathaway nchini Marekani ambayo kwa ujumla yameajiri watu zaidi ya 360,000.

Akiwa na miaka 11 alianza kuwekeza kwenye kampuni ya Cities Service Preferred akianza kwa kununua hisa tatu tu ambapo hisa moja iliuzwa kwa dola 38. Akauza hisa hizo kwa faida kiduchu kwa kuuza hisa moja kwa dola 40, baada ya thamani ya hisa za kampuni hiyo kushuka mpaka dola 27, baadae akajuta baada ya thamani ya hisa kupanda mpaka dola 200.

Anasema majuto haya ndiyo yaliyomsukuma kufikiria zaidi uwekezaji na kuwa mmiliki wa kampuni kubwa usoni. Kufika huko ilipaswa awe na mtaji wa kuanzia, na kazi yake ya kusambaza magazeti ilikua moja ya njia ya kumfikisha alipofika sasa.

5: Salim Said Bakhresa

Ingawa si bilionea katika orodha tajika ya Forbes, lakini historia yake inamleta kwenye kundi la watu matajiri walioanza kufanya kazi za kawaida kabisa mpaka kuwa matajiri wakubwa Afrika. Ni milionea tajika Afrika akizaliwa visiwani Zanzibar, Tanzania.

Kama ilivyo kwa watoto wengi wa Tanzania na vijana wengi wa nchi hiyo, hupitia kufanya kazi nyingi za kawaida kutokana na uchumi uliopo na mazingira ya nchi hiyo. Bakhresa alianza kuuza mabaki ya mazao ya baharini tu yanayopatikana kwa wingi hata sasa kwenye fukwe za bahari katika maeneo ya Zanzibar, Dar es Salaam na Mombasa.

Bakhresa hakulala na kuamka tajiri bali alianzia mbali kuusaka utajiri wake. Alianza kwa kushona viatu, akauza urojo na viazi kabla ya kufungua mgawaha mdogo lakini leo makampuni yake kwenye sekta ya Usafirishaji, Vinywaji, vyombo vya habari, maji, vyakula, viwanda vya nguo, hoteli na vitu vingine ambayo yameajiri zaidi ya watu 2,000 na kuingiza mabilioni ya fedha.

Makampuni ya Said Salim Bakhresa & Co. (SSB), yananufaisha zaidi ya watu 6,000 kwa ajira rasmi na zisizo rasmi katika nchi za Afrika Mashariki. Bidhaa zake za makampuni yake zinapatikana karibu nchi sita za Afrika Mashariki.



# MIKAKATI YA MIRADI YA KIMAENDELEO... NI DK. SAMIA SULUHU HASSAN KUMALIZA KAZI

NA MWANDISHI WETU



CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimepitisha azimio la kumteua Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea wa nafasi ya urais katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika baadae mwaka huu.

Azimio hilo limepitishwa na Mkutano Mkuu wa CCM ambao ndiyo chombo cha mwisho cha maamuzi ya uteuzi wa mgombea wa tiketi ya urais kupitia chama hicho. Chama hicho pia kimempitisha Dkt. Hussein Mwinyi kugombea Urais kwa upande wa Zanzibar.

Uamuzi huo umefanyika mapema kuliko kawaida, na katika mkutano ambao awali haukupangwa kufanya maamuzi hayo katika ajenda zake. Mkutano huo ulikuwa na ajenda kuu moja ya kupitisha jina la Makamu wa Mwenyekiti (Bara) ambapo mwanasiasa mkongwe Stephen Wasira alipitishwa kushika wadhifa huo jana Jumamosi.

Baadhi ya wajumbe waliokuwa wakitoa michango yao juu ya utekelezwaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM walipendekeza mkutano huo kuwapitisha Rais Dkt. Samia na Rais Dkt. Mwinyi kama wagombea wa urais kutokana na maendelea walioyasimamia.

Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kujipambanua vyema katika utendaji wake kazi, imebainika miradi ya maendeleo iliyosajiliwa mwaka jana inatarajiwa kuzalisha ajira kwa Watanzania 212,293.

Hii ni kutokana na miradi 901 iliyosajiliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kuanzia Januari hadi Desemba 2024 kulinganisha na miradi 526 katika kipindi hicho mwaka 2023.

Miradi hii iliyosajiliwa mwaka jana inatarajiwa kuzalisha idadi hiyo ya ajira kwa Watanzania, kulinganisha na ajira 137,010 zilizozalishwa mwaka 2023.

Taarifa iliyotolewa na Waziri wa Nchi, Mipango na Uwekezaji Prof. Kitila Mkumbo ilitaja pia mikoa iliyoongoza kwa kuvutia uwekezaji ni Dar es Salaam, Pwani, Arusha na Dodoma.

Prof. Mkumbo alisema, Dar es Salaam ilifanikiwa kusajili miradi 356, Pwani ikisajili miradi 166, Arusha miradi 64 na Dodoma ikiwa na miradi 47 ambayo ni sawa na asilimia 70.3 sawa na jumla ya miradi 633 iliyosajiliwa katika mikoa hiyo.

> *Mpango ataendelea na majukumu yake kama Makamu wa Rais mpaka uchaguzi utakapofanyika, sawia na Nchimbi ambaye ataendelea na majukumu yake ndani ya chama kwa sasa.*

Alitaja sekta tano zinazoongoza kwa kusajili miradi mingi ya uwekezaji kuwa ni uzalishaji viwandani, usafirishaji, ujenzi wa majengo ya biashara, utalii na kilimo.

"Mwaka 2024 tunaweza kuutangaza ni mwaka bora zaidi katika sekta ya uwekezaji Tanzania, kutokana na ukweli kwamba ndio mwaka ambao TIC ilisajili miradi mingi zaidi ya uwekezaji (miradi 901) tangu Tanzania ianzishe kituo hiki," alisema Prof. Mkumbo. Miradi hii imevutia jumla ya mitaji ya Dola za Kimarekani bilioni 127, kiwango ambacho hakijawahi kufikiwa tangu kuanzishwa kwa TIC.

Alisema kuwa, mafanikio hayo ni ushahidi wa dhamira thabiti ya Rais Dkt. Samia katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

"Hii ni miradi mingi zaidi kuwahi kusajiliwa na Rais Samia ameonyesha maono makubwa tangu ahadi yake aliyoitoa Aprili 2021 alipohutubia Bunge," alisema.

Katika mkutano huo wa CCM, Rais mstaafu Jakaya Kikwete, akizungumza kama mmoja wa wazee wa chama, alisisitiza kuwa CCM ina mamlaka ya kujichagulia mgombea wao kwa wakati wowote.

"Hili lipo ndani ya uwezo wetu, kuamua muda wowote, kwamfano wenzetu (wa Swapo) Namibia wao wanafanya uchaguzi kumpitisha mgombea wao mwaka mzima (kabla ya uchaguzi). Sasa na sisi tunaweza kuamua. Jambo la Msingi azimio lipite na tupate ushauri wakisheria ili uendane na matakwa ya tume ya uchaguzi."

Hii ni mara ya kwanza kwa CCM kupitisha wagombea wa nafasi za urais mapema katika mwanzo wa mwaka na katika kikao ambacho ajenda yake mahsusi haikuwa hiyo. Kawaida, maamuzi hayo hufanyika miezi michache kabla ya kuanza kwa kampeni rasmi za uchaguzi mkuu.

Rais Dkt. Samia pia amemteua Katibu Mkuu wa CCM Emmanuel Nchimbi kuwa mgombea mwenza wake katika uchaguzi mkuu utakaofanyika baadae mwaka huu.

Nchimbi ni mwanasiasa mwandamizi na ameshika nafasi mbali mbali ndani ya CCM na serikali yake kwa miongo mitatu iliyopita. Amewahi kushika nafasi ya Waziri wa Mambo ya Ndani katika serikali ya Kikwete na aliteuliwa kuwa balozi na hayati John Pombe Magufuli na kuiwakilisha Tanzania nchini Brazil na baadae Misri.

Kwa mujibu wa Rais Dk. Samia, Makamu wa Rais wa sasa Philip Mpango alimuomba apumzike na ameridhia na ndio maana amemteua Nchimbi.

Mpango ataendelea na majukumu yake kama Makamu wa Rais mpaka uchaguzi utakapofanyika, sawia na Nchimbi ambaye ataendelea na majukumu yake ndani ya chama kwa sasa.

Marais wote wawili Dkt. Samia na Dkt. Mwinyi wanamaliza awamu zao za kwanza za uongozi mwaka huu. Na kwa mujibu wa utamaduni wa chama hicho, marais walio madarakani huwa hawapatiwi ushindani katika kupewa tiketi ya kugombea urais kwa awamu ya pili.

Rais Samia aliingia madarakani mwezi Machi 2021 mara baada ya kifo cha aliyekuwa rais wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli. Aliingia madarakani kwa mujibu wa katiba akiwa ndiye mrithi wa urais, kwa nafasi aliyokuwa nayo kipindi hicho ya Makamu wa Rais.

# YANGA YAAPIA MAKUBWA

>> Inatoka uk. 16

safari. Kamwe amesema maumivu wanayopata kwa kuondolewa kwenye makundi wanaweza kuhisi makubwa na mazito, wanatakiwa kutumia nafasi hii kujiuliza na kujipanga kwa ajili ya kutetea mataji ya Ligi Kuu na Kombe la Shirikisho la FA.

"Tukipoteza makombe yetu tuliyopata msimu uliopita, maumivu haya yatakuwa maumivu makali mara mbili au zaidi. maumivu haya yawe darasa na sehemu ya kupambana kufanya vizuri, tusije kuumia zaidi, tumegundua furaha yetu inawaumiza wapinzani wetu, basi tushikamane," alisema.

Kamwe alisema, sasa nguvu na akili zao wanatakiwa kuelekeza katika michuano iliyopo mbele yao ya Ligi Kuu na michuano ya kombe la FA kuhakikisha wanafanikiwa kutetea mataji hayo. "Tunahitaji kufanya vizuri katika michezo yetu ya ligi kukusanya alama tatu kila mechi na kurejea kwenye nafasi yetu ya kuongoza ligi na kufanya vizuri michuano ya FA," alisema Kamwe. Yanga inatarajiwa kushuka dimba la KMC Complex, kwenye mchezo wa michuano ya Kombe la Shirikisho la FA dhidi ya Copco FC, utakaochezwa, Jumamosi, Januari 25.



# MO SALAH FEDHA ZAMNGOJA

RIYADH, SAUDIA

MSHAMBULIAJI wa Misri Mohamed Salah, 32, anatazamiwa kupewa ofa ya pauni milioni 65 ili kumshawishi kuondoka Liverpool kuelekea Saudi Arabia msimu wa joto.

Nao Real Madrid wameachana na harakati zao za kumnasa mlinzi wa Liverpool Trent Alexander-Arnold, 26, na watarejea kumchukua mlinzi huyo wa Uingereza msimu wa joto.

# WALISEMA SIMBA HAIFIKI ROBO ... HAPAWAPI?

NA MWANDISHI WETU

ACHENI kumaliza maneno. Acheni kuropoka. Acheni muda uongee. Nini sasa? Tumefika robo au bado? Acheni hizo. Simba ndiyo waanzilishi wa hizi kazi.

Nilishasema, kufika robo fainali haiwezi kuwa kazi ngumu kwa Simba. Tumefika sasa, ongeeni mambo mengine. Najua wapo waliosema hatufiki. Bado wapo au wameshaondoka?

Wamejificha wapi tena hao jama zetu? Ngoja tuulizane tu. Mwisho wa siku, mambo yamekuwa magumu kwao. Kibarua walichonacho ni kizito. Unafikiri ni rahisi kumfunga Mwarabu akiwa anahitaji pointi moja tu? Ngojeni muone sasa. Zile dua zao zinarudi kwao.

Sisi kwetu tumeshamaliza. Tunasubiri atakayepita mbele yetu katika hatua inayofuata ya nusu fainali. Tutapiga yeyote atakayekatiza mbele yetu. Hatutaki ujinga.

Nilishasema, Simba iliyofika robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika haiwezi kusumbuliwa na timu za Kombe la Shirikisho. Safari hii, tunataka kuionesha dunia kuwa Simba ni timu kubwa.

Niwaambie tu; Simba hii ndiyo timu pekee ya Tanzania itakayobaki kwenye michuano ya kimataita. Nawaambia ukweli. Tunautaka ubingwa wa Shirikisho.

Tulianza kwa kusuasua lakini sasa timu imeshakaa vizuri. Fadlu ameshaseti mitambo yake na sasa gari limewaka. Gari limewaka.

Tusisahau, ubingwa wa Ligi Kuu Bara nao tunautaka. Safari hii, ni nje na ndani. Hatuachi kitu. Hata kingekuwa kikombe cha kahawa, tungebeba tu.





# MAVOKO ashtushwa, taarifa za kuomba kurudi WCB

NA MWANDISHI WETU

MSANII wa Bongofleva, Rich Mavoko amesema alishtushwa na taarifa zilizokuwa zinasambaa mtandaoni kuwa ameomba msamaha ili arudi kufanya kazi na WCB Wasafi.

Mavoko ambaye alitoka WCB mwaka 2018, alisema alisikia taarifa hizo za kizushi kupitia mdogo wake lakini baada ya kufuatilia aligundua ni uongo hivyo akapuuzia.

"Sijawahi kujaribu kuomba msamaha na hakuna kitu kama hicho, bora nivae shati lililochanika kuliko kutembea tumbo wazi, kikubwa naomba mashabiki zangu waendelee kunipa sapoti kupitia wimbo wangu mpya Usizuge." amesema Mavoko.

# Idris Sultan: Wakenya hawajatuzidi, ila wametuwahi kidogo

NA MWANDISHI WETU


MCHEKESHAJI na Mwanamitandao maarufu wa Tanzania Idris Sultan, ametolea ufafafanuzi dhana iliyopo kuhusu tasnia ya Sanaa nchini Tanzania kuzidiwa kimaendeleo na tasnia ya Sanaa chini Kenya kwakua Kenya wanazo kazi nyingi za kimataifa kuliko Tanzania, ambapo jibu lake likawa ni 'Kind off'.

Idris alitolea maelezo dhana hiyo kwa kuweka wazi kuwa kwa kiwango flani Kenya wamesogea lakini bado hawajaiacha tasnia ya Sanaa ya Tanzania, aliyasema hayo alipoulizwa na chombo The chanzo, kwanini Kenya ina filamu nyingi kwenye Mtandao wa Netflix na channel ya 'Showmax' kwa upande wa Afrika Mashariki kwani wao wanatuzidi nini?

"Hawajatuzidi leo kwa bahati mbaya, wametuzidi zamani kidogo na hiyo zamani ndio ime-determine leo yao na ilikua ni lugha (kiingereza) na sio kwenye kutuzidi labda kwenye kuongea, bali wamekitumia kwenye kazi zao za kisanaa, na Kenya hawaongei kiingereza tu au kiswahili tu, bali wanachanganya kiswahili na Kiingereza, hii inawasaida kuwa na mfanano na Mataifa mengine. Sasa unapoingia kwenye majukwaa ya kimataifa kama Netflix na Showmax ukija kutengeza maudhui, unataka uweke maudhui ambayo watu wengi katika mataifa tofauti wanaweza kuyaelewa na hapo ndipo lugha inaposaidia' amesema Idris

Ambapo pia ametilia mkazo kuwa licha ya Wakenya kuwahi kufanya mambo makubwa kwenye sanaa mbele ya Tanzania, kwa sasa hali ni tofauti kwa sababu ukubwa wa vipaji, wasanii, uwekezaji pamoja na vipaji Tanzania iko mbele ya Kenya.

"Kwa hiyo wao Kenya, tuseme tu walituwahi, lakin kwasasa hivi ukisema utuweke kwenye mzani mmoja na unangalie ni wapi wametuzidi kwenye Sanaa Kwa ujumla, kuanza ujuzi, vipaji na ubunifu ni wazi sisi tuko juu yao pakubwa sana kwenye sanaa Kwa ujumla wake na sio muziki wala filamu tu peke yake,"aliongeza.



# DRAKE AFICHUA SIRI YA MAFANIKO YAKE



LOS ANGELES, MAREKANI

SUPASTAA wa muziki wa Hip hop, Drake, amesema siri ya mafanikio yake ni kujifunza kutoka kwa waliofanikiwa.

Drake mwenye umri wa miaka 38, amesema tangu alipokuwa mdogo, alipenda kufuatilia maisha ya mastaa na kuvutiwa na hatua zao kwenye maisha.

Mshikaji huyo mzaliwa wa Toronto, alianza rasmi safari yake ya muziki mwaka 2006 kupitia 'mixtape' yake ya 'Room for Improvement.'



UK. 15


tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora

Tanzania BORA

# MICHEZO

ALHAMISI Januari 23, 2025

Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz


# YANGA YAAPIA MAKUBWA




NA ASHA SEKEFU

YANGA imesema, kwa sasa hasira zake zote zinarejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kuondoshwa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambapo walifika hatua ya makundi.

Kutokana na kuondolewa huko, Yanga imesema ina maumivu makubwa kwani pamoja na kutimiza lengo lao la kufika makundi katika hatua hiyo, lakini kutolewa huku wakiwa na nafasi ya kusonga mbele imewaumiza mno. Meneja Habari na Mawasiliano

Yanga, Ali Kamwe amekiri maumivu ya kutolewa kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwao ni darasa tosha na sehemu ya wamejifunza nini cha kufanya, ili wasije kuumia zaidi mbele ya

Inaendelea Uk.14

# Manchester United kuna vimeo wanane

MANCHESTER, ENGLAND

WAPO NANE! Imeelezwa Manchester United kuna wachezaji nane ambao hawana sifa za kuichzea timu hiyo, huku ikidaiwa hata ufikaji wao hapo inabidi 'waulizwe kwa makini' wale waliowaleta.

Kauli hiyo imetolewa na mchezaji wa zamani wa timu hiyo, aliyepita katika mafanikio makubwa Paul



Scholes, ambaye alisema wachezaji hao wanapaswa kuuzwa na timu kutengenezwa upya.

Paul Scholes amesema, wachezaji hao nane wanatakiwa kuuzwa kwa haraka mno kabla ya dirisha la sasa la usajili kufungwa, la sivyo timu itaendelea kufanya vibaya katika kila mechi.

Scholes, ambaye alicheza michezo 714 akiwa ndani ya kikosi hicho, bila kuwataja alisema wachezaji ni mzigo

Inaendelea Uk.14

# SIMBA: TUNAOGOPWA AFRIKA

NA ASHA SEKEFU

WACHEZAJI Simba wametoa yao ya moyoni na kusema, kufanikiwa kutinga robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, huku wakiongoza kundi lao kumeifanya timu hiyo izidi kuogopwa zaidi barani Afrika.

Akizungumza kwa niaba yao, Nahodha wa Simba, Mohammed Hussein `Zimbwe Jr', amesema kumaliza kinara wa kundi kwenye michuano kombe la Shirikisho Afrika kumewapa nafasi ya kumewafanya wazidi kuwa tishio barani Afrika.

Simba hatua inayofuata ya robo fainali inatarajiwa kucheza na kati ya Stellenbosch ya Afika Kusini, Al Masry ya Misri au Asec Mimosa ya Ivory Coast.

"Kwa `Level`ya Simba ilipofikia sio kuogopa timu au mpinzani yoyote anayekuja mbele yetu, siku zote unapomaliza nafasi ya juu unatengeneza nafasi ya mpinzani kukuogopa," amesema.

Zimbwe Jr amesema baada ya kufanikiwa sasa wanahitaji kuona Simba inaendelea kufanya vizuri katika hatua inayofuata na kucheza nusu fainali.

"Simba bado haijawa imara kama ilivyokuwa misimu mitatu au minne, lakini taratibu tunarudi kwenye ubora wetu kwa kuwa tishio kwa mashindano ya ndani na nje," amesema.

